JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

NOVEMBA 2025



CamScanner

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**NJOMBE GIRLS' SECONDARY SCHOOL,**

**S.L.P 1095,**

**NJOMBE.**

**01/11/2025**

Ndugu mzazi/mlezi wa mwanafunzi ………..........................................................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA NJOMBE (NJOMBE GIRLS' SECONDARY SCHOOL), HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE, MKOA WA NJOMBE MWAKA WA MASOMO 2026.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2026.

Shule ya Sekondari ya Wasichana Njombe (Njombe Girls' Secondary School) ni shule ya **BWENI KITAIFA** na inapatikana Mkoa wa Njombe, Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, tarafa ya imalinyi, kata ya Ulembwe, kijiji cha Usalule. Shule ipo umbali wa kilometa 20 kutoka Njombe mjini barabara ya Makete. Usafiri wa mabasi, noa au probox unapatikana muda wote wa mchana kwa nauli ya shilingi **2000** tu ukitokea kituo cha Stendi ya mabasi ya zamani ya Njombe.

Muhula wa kwanza wa Masomo unaanza tarehe **12/01/2026** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia **05/01/2026** hadi tarehe **10/01/2026** kuanzia saa **2:30** asubuhi hadi saa **10: 30** jioni. Na masomo yatanza rasmi tarehe **12/01/2026** tunaomba mzazi mwanafunzi awahi kufika ili tuendane na mipango ya ufundishaji wa shule.

**2.** KAULI MBIU YA SHULE: ***"Dream big, aim high and work hard to achieve more" ikiwa na maana ya "Ndoto kubwa, malengo ya juu na fanya bidii kufikia zaidi."***

Kauli mbiu hii ndiyo dira yako utakapokuwa hapa shuleni kwa kipindi chote cha masomo yako. Utatakiwa kuitafakari daima kwa vitendo, hivyo utatakiwa kuwa na tabia njema uwapo shuleni na uhudhurie masomo yote ukijifunza kwa bidii.

**3. MAHITAJI MUHIMU KWA WANAFUNZI**

a.) Sare za Shule

(i.) Sare za darasani:

- Suruali 02 ndefu rangi ya kijivu mpauko (light grey) namba moja. zisizo za kubana mwili.
- Vigauni viwili (02) rangi ya kijivu mpauko (light grey), mshono wa rindaboksi. Mshono kuanzia begani hadi chini ya goti. Zipu iwekwe pembeni chini ya kwapa.
- Sweta za darasani mbili 02 za rangi ya Light Grey (Kijivu Mpauko) mshono wa V shingoni yenye nembo yanapatikana shuleni kwa **tsh. 15,000/=kwa moja.**



CamScanner

- Mashati mawili (02) mikono mirefu kitambaa cha Tomato original.
- Pull-neck nyeupe mbili (02) au zaidi (pure plain white)
- Kofia za kuvaa darasani (mizula) rangi ya kijivu mpauko (light grey) inapatikana shuleni kwa **Tsh.5000/=**
- Raba nyeupe jozi mbili (02) za darasani. **(AIR FORCE)** ISIWE NA MCHANGANYIKO WA RANGI
- Soksi nyeupe jozi nne (04) au zaidi **(Free size)**
- Hijabu (kijuba) nyeupe isiyo na urembo ifunike kifua cha mwanafunzi iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama. (**kwa WAISLAMU TU).**




**(ii.) Sare za kushindia (shamba dress).**

- Sketi ndefu mbili 02 za rangi ya Dark Blue namba moja (01) **ndefu mpaka kwenye kisigino** mshono wa rinda ya kawaida. (Mshono umeambatanishwa)
- T-shirt ya kola (Dark blue, plain). Yenye nembo ya shule inapatikana
- Tracksuit mtelezo rangi nyeusi yenye mistari myeupe pembeni isiyo na kofia.
- Raba nyeusi za kushindiana michezoni.
- Masweta ya kushindia 02 ya rangi ya Dark Blue. Yanapatikana shuleni kwa tsh **15000** kwa moja.
- Gum buti rangi nyeusi .
- kofia za kushindia mizula rangi ya dark blue inapatikana shuleni kwa **tsh 5000** kila mmoja.
- Ndala nyeupe (umoja) **na siyo aina nyingine yoyote ya yebo au simple.**
- Hijabu (kijuba) dark bluu isiyo na urembo ifunike kifua cha mwanafunzi iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama. **HII NI KWA WAISLAMU TU.**






CS CamScanner

**(iii) sare za michezo.**

- Tisheti ya rangi ya blue bahari (light blue)
- Bukta ya ngi ya blue bahari (light blue)
- Stocks ndefu rangi nyeusi kwaajili ya kutanguliza ndani kabla ya bukta. (skin tight)

**b.) Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari madogo(Msomi) 12
ii. Counter book Q4 12 au zaidi
iii. Graph pad 02 au zaidi.
iv. Ream 2 (A4) ya Karatasi kwa mwaka;
v. Vitabu vya masomo yote anayosoma (Vya TIE).
vi. Godoro dogo la futi 02½ x 6
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink
viii. Blanket **nzito 01**,
ix. Spring file mbili(2).
x. Mto mmoja (01)
xi. Foronya rangi ya pink 02,
xii. Chandarua nyeupe 01.
xiii. Nguo za ndani za kutosha kuanzia tano (05) na kuendelea.
xiv. Sanduku la chuma (tranka) lenye kufuli na funguo.
xv. Vyombo vya chakula vyote viwe vya **alminium[bati]**
  - *Sahani yenye partion moja,*
  - *Bakuli moja ,*
  - *Kijiko kimoja 01 na Kijiko uma.*
  - *Kikombe kikubwa cha nusu lita*

xvi. Ndoo 2 (lita Kumi moja na lita 20 moja) zenye mifuniko. Iwe ya mafuta au amboni.
xvii. Doti moja ya Kanga au kitenge na taulo.
xviii. Mafuta ya kupakaa yanayohitajika ni mgando na sio ya kujichubua. Mfano carolite, cream n.k

**VIFAA VYA USAFI.**

a) Jembe lenye mpini.
b) Sabuni ya maji ya chooni lita 5 (careline).
c) Squeezer (mopa).
d) Slasher (kwanja).
e) Ufagio wa chelewa mmoja.

**4. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.



CamScanner

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MAAGIZO MUHIMU:**

- ❖ Ni wajibu wa kila mwanafunzi kufaulu akiwa NJOMBE GIRLS' sekondari na ufaulu unaotakiwa ni **daraja** la **kwanza pointi 7-9.** Mwanafunzi ambaye atashindwa kupata daraja hilo likizo atalazimika kubaki shuleni kujisomea na kufuta alama alizopata ambazo hazitakiwi.
- ❖ Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na bima ya afya ya **NHIF**, na kama hana mwanafunzi anatakiwa aje na tsh **50,400** ili aweze kutengenezewa bima yake kwa mwaka. Hii inapunguza gharama za matibabu akiwa shuleni.
- ❖ Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na vitabu vya masomo yafuatayo;( **ni lazima)**

*i. <u>Kiswahili</u>*
*ii. <u>English language</u>*
*iii. <u>Basic mathematics</u>*
*iv. <u>Business studies</u>*
*v. <u>Geography</u>*
*vi. <u>Historia ya Tanzania na maadili</u>*
*vii. <u>Physics</u>*
*viii. <u>Chemistry</u>*
*ix. <u>Biology</u>*
*x. <u>History</u>*

- ❖ Kila mwanafunzi anatakiwa awe na account ya bank ya CRDB atakayotumia mzazi au mlezi kumtumia fedha za matumizi mwanafunzi akiwa shulen. Kama hana atatakiwa kuja na tsh.10000 ili aweze kufunguliwa akaunti.

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i.) Wizi
ii.) Kutohudhuria masomo darasani
iii.) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv.) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v.) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi.) Kusuka nywele.
vii.) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii.) Uvutaji wa sigara;
ix.) Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;



CS CamScanner

x.) Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi.) Kusababisha mimba;
xii.) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii.) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xiv.) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xv.) Kudharau Bendera ya Taifa.
xvi.) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
xvii.) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

i.) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.
ii.) Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
iii.) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.
iv.) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v.) Cheti cha kuzaliwa (nakala moja 01)

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. **TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

| **MAWASILIANO** | |
|---|---|
| **MKUU** | **0753 561 528** |
| **MAKAMU** | **0741244721** |
| **MATRONI** | **0741244716 / 0741244717** |
| **BARUA PEPE** | **njombegirlssecondaryschool@gmail.com** |

**KARIBU SANA NJOMBE GIRLS' SEKONDARI.**

..............................

**EDITOR HEDWICK JOHN.**

**MKUU WA SHULE.**

HEAD MISTRESS
NJOMBE GIRLS SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 1095
NJOMBE

**OFISIYA RAIS TAMISEMI HALMASHAURI YA WILAYA YAWANGING'OMBE SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA NJOMBE (NJOMBE GIRLS' SECONDARY SCHOOL)**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI.**

**A: TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI (Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)**

(i.) Jina kamili …………………………………………….

(ii.) Tarehe kuzaliwa ……………… ……………………………………………

(iii.) Kabila ………………….. ……………………………………..…………….

(iv.) Dini na dhehebu ……………… ……………………………………………..

(v.) Mwaka wa masomo …………………………………………………………

(vi.) Shule nitokayo ………………. …………………………………………..…

(vii.) Mahali ninapoishi ……………. …………………………………………..…

(viii.) Mkoa ………………. ……………………………………………………..

(ix.) Anwani ……………….. ………………………………………………………

(x.) Jina la Baba/Mlezi……………………………….Kazi yake ………………………

(xi.) Wazazi/Walezi wanaishi wapi………………….pamoja/wametengana…………………

(xii.) Anwani ya mzazi/mlezi……………………………... Simu …………………………...

(xiii.) Wakati wa likizo nitakuwa kwa (mtaje) ……………………………. wapi……………

(xiv.) Nathibitisha kuwa taarifa hapa juu ni za kweli na sahihi

***Sahihi ………………………… Tarehe …………………..***

**KUKUBALI NAFASI**: Mimi ……………………………………………………….nimesoma maagizo kwa makini na kuzielewa taratibu za shule na nipo tayari kuzifuata. Hivyo nakubali nafasi niliyopewa na nitafika shuleni tarehe zilizopangwa.

B. **IJAZWE NA MZAZI/MLEZI**

Mimi ……………………………………………ambaye ni ……………. wa mwanafunzi huyu nimesoma kwa makini maelekezo pamoja na sheria za shule.Nipo tayari ajiunge na shule hii, ninaahidi kumtolea ada, michango na mahitajiyote ili aweze kupata elimu yake vizuri. Aidha nitasaidiana na walezi wa shuleni katika kumlea mwanafunzi huyu katika maadili mema na kuitika wito wa kufika shuleni pale nitakapohitajika. Anwani yangu ya kudumu ……………………… Simu ……………………….. Nikipata uhamisho ama kubadilisha makazi nitaijulisha shule kwa maandishi. Ndugu zangu wanaweza kumtembelea mwanafunzi akiwa shuleni siku za wageni ni;

1. …………………………..Uhusiano kwa mwanafunzi ……………. Simu ………………..……
2. …………………………...Uhusiano kwa mwanafunzi ……………. Simu ………………….…
3. … ……………………....Uhusiano kwa mwanafunzi ……………. Simu ……………….……

Nathibitisha taarifa nilizotoa ni sahihi na kweli.

Sahihi ya mzazi/mlezi ……………………..…Tarehe………………



CamScanner

**NJOMBE GIRLS SECONDARY SCHOOL**

**STUDENT'S MEDICAL CERTIFICATE**

To be completed by a Government Medical Officer and returned to the Headmistress of Njombe Girls secondary Secondary School,P.O. Box1095 Njombe .

To Medical Officer

……………………………………………………………………………………………………

REFER:

**STUDENT'S NAME: ………………………………………………………………………**

**FORM: ……………………………………………………………………………………**

**AGE:**

**…………………………………………………………………………………..**

**SEX: ………………………………………………………………………………………..**

Please, examine the student mentioned above and comment on her health by responding to the following items. Kindly put a tick or cross in front of either Yes or No as you find appropriate.

Thank you in advance. .................................. Does the student have problems in connection with:

• Sight? Yes/No If yes state……………………………………………………… …………………

•Hearing? Yes/No If yes state…………………………………………………………………………

• Speech? Yes/No If yes state…………………………………………………………………………

• TB? Yes/No If yes state…………..…………………………………………………………………

• Blood Pressure Yes/No If yes state…………………………………………………………………

• Any Physical disability? Yes/No If yes state………………………….…………………………..

Do you, therefore, recommend the said student medically fit for studentship at this school? Yes/No If no please state the reasons…………………………………………………………………………………

**Name of Medical Officer…………………………………………………..signature………………………**

**Designation & Stamp………………………………Date……………………………………………..**